# Ukadiani Sio Uahmadiyya
## Majibu ya
## Hakika Ya Ukadiani

Mwandishi

Sheikh Muhammad Munawwar H.A.

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

**Ukadiani Sio Uahmadiyya**
**Majibu ya**
**Hakika ya Ukadiani**

Mwandishi:
Sheikh Muhammad Munawwar H.A.


| | |
|---|---|
| Chapa ya Kwanza: | 1974 |
| Chapa ya pili: | 1975 |
| Chapa ya tatu: | 1982 |
| Chapa ya nne: | 2020 |


© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031
Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover design: Farhan Naseer

ISBN: 978-1-84880-527-9
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# NENO LA MBELE

Mpinzani mmoja wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya alitoa kijitabu chake mnamo mwaka 1974 kwa lengo la kuwapoteza wasomaji wake. Haraka sana Maulana Sheikh Muhammad Munawar H. A. akamjibu vya kutosha. Hatukupata habari kwamba huyo mpinzani, Bwana Abdillah Nasir wa Mombasa akatoa jawabu la majibu ya Maulana Sheikh Muhammad Munawwar.

Kitabu chetu — Ukadiani Sio Uahmadiyya — kilimalizika haraka na kikachapwa mara ya pili mwaka 1975.

Hii mkononi mwenu ni chapa ya mara ya nne. Bila shaka kitabu hiki kimewanufaisha watafutao haki.

Twakichapisha mara ya tena ili wale wasiopata kukisoma mpaka sasa wakitalii ili kujua namna wapinzani wa Ahmadiyya wanavyowalaghai watu, na wajitahadhari. Ili kujua uhakika wa Ahmadiyya wasomaji watukufu wanashauriwa kusoma vitabu vilivyotolewa na Jumuiyya hii kwa Kiswahili.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 27.02.2020

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [1]

# UKADIANI SIO UAHAMADIYYA

Majuzi tumeletewa kijitabu kimoja kutoka Afrika ya mashariki kilichoandikwa na Abdillahi Nassir wa Mombasa na kuenezwa na National Union of Kenya Muslims na Ansaar Muslims Mission, P.O. Box 85529, Mombasa. Kitabu hiki kimepewa jina Hakika ya Ukadiani. Tumekisoma tupate kuelewa uchunguzi uliofanywa na mtaalamu huyu wa Mombasa na tunasmea kwa masikitiko mengi kwamba mwandishi wake hakupenda kudhihirisha haki, bali amejaribu kuificha na kuionyesha sivyo ilivyo. Hatusemi kwamba Abdillahi Nassir hana ujuzi wowote juu ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa maana amekuwa pamoja na wabashiri wetu muda mrefu na bila shaka amepata kusoma vitabu vingi vilivyoenezwa na Jumuiya hii kwa Kiswahili na Kiingereza. Jambo hili limezidisha huzuni yetu kweli kweli.

## Nia yake si Njema

Huyu Bwana kama angekuwa na haja ya kueleza haki angesoma kwanza vile vitabu ambavyo vinapatikana kwa wingi katika lugha aliyofundishwa na mama yake. Na ikiwa alikuwa amepata tatizo lolote juu ya imani yetu au mafundisho ya jumuiya ya Ahmadiyya ilimlazimu

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingiwa Rehema na Ukarimu.

aonane na wabashiri wetu au wanachama wa Jumuiya hii ambao wako Mombasa, Nairobi, Kisumu na sehemu nyinginezo za Kenya. Pia alikuwa na nafasi ya kuandikiana na masheikh wa Kiahmadiyya au ndugu wengine wanaohusiana na Jumuiya, nao wangekuwa na furaha kuu katika kumjibu na kumweleza uhakia ulivyo. Kwa kweli, msomaji wa vitabu kama Abdillahi Nassir asingekosa majibu ya maswali yake katika vitabu vyetu na magazeti yetu na Tafsiri na Maelezo ya Kurani Tukufu yaliyotolewa nasi tangu miaka zaidi ya 20. Lakini hakutafuta uhakika wa mambo ndani ya vitabu na magazeti yaliyoandikwa kwa Kiswahili. Marejeo aliyoandika ndani ya kijitabu chake yametokana na vitabu vilivyoandikwa Kiurdu. Na wasomaji wetu wanafamahmu sana ya kuwa mtaalamu huyu haelewei lugha hiyo hata akajua nini muradi wa maneno aliyoyaandika katika utungo wake. Basi tunasema kwamba yeye hana vitabu hivyo alivyoandika majina yake ndani ya makala yake. Sio kwamba vitabu hivyo havipatikani kwake, bali tunasema ya kuwa hata hakuviona wala hakuvigusa kwa mkono wake. Je, mtu mwenye hali hiyo tumwiteje? Ni mwelezaji uhakika? Kama angekuwa na nia ya kuuelewa uhakika, kwa nini asichukue maneno ndani ya vitabu vinavyoenezwa kwa Kiswahili tangu miaka 30? Kwa nini akimbilie vitabu asivyoviona katika maisha yake yote hata mara moja?

Hili tu laonyesha kamba si mtafuta ukweli wala si mwelezaji uhakika. Ni mtu tu aliyehongwa na jamaa

fulani kueleza uongo katika watu wanaomjua kuwa ni mwanachuoni na mtu mjuzi. Na sasa watu hao watatahayari watakaposoma kwamba vitabu vilivyotajwa katika kijitabu chake ni karibu vyote vya Kiurdu na mtu wao hana ujuzi wa lugha hiyo asilani. Itaonekana kwamba National Union of Kenye Muslims na Ansaar Muslim Mission vimefanya kazi isiyo na maana. Ni kazi isiyoweza kutegemewa na yeyote yule. Mwulize mwenyewe Abdillahi Nassir, je ameona vitabu alivyovitaja kitabuni mwake? Je, anakielewa Kiurdu? Ya nini, basi, kupoteza fedha juu ya kazi isiyo na thamani hata ya pesa mbili? Je, hamna shughuli nyingine ya maana yenye kuwanufaisha Waislamu? Au hamna huruma juu ya fedha msiyoichuma ninyi kwa jasho lenu? Hakika, viongozi waaminifu sasa hawapatikani kwenu, waila wasingechezea fedha ya Waislamu kwa fujo vile bila kuona kizazi cha Kiislamu kimepungukiwa nini na mahitaji yao kwa wakati huu ni vifaa gani.

## Huu sio Wakati wa Kutengana

Tena kijitabu hiki hakitambui wakati huu ni wa kutengana au wa kuungana. Tusilaumu kitabu, bali tuelekeze lawama yetu upande ule ule unaostahili kulaumiwa. Waislamu wa dunia nzima hivi sasa wako mbioni kuleta umoja na upendo baina ya Waislamu wenyewe. Hapa Pakistan kunapangwa mkutano wa viongozi wote wa seikali za Kiislamu ili washauriane juu ya mambo yenye kuwaleta karibu na ndugu zao. Taabu na shida ambazo zimewasonga Waislamu wa ulimwengu

huu mzima zinamchochea kila Mwislamu mwenye nia safi afikirie njia za kuleta umoja wa Waislamu, kwani umoja ndio dawa ya shida hizi zenye kusumbua na kuhangaisha roho za Waislamu. Lakini tuseme nini juu ya viongozi wa Waislamu katika nchi ya Kenya. Hawakumbuki jambo lolote la heri kwa ndugu zao Waislamu ; bali wantafuta njia za kujaza uongo na chuki na fitina bongo zao na akili zao na fikira zao. Viongozi hao wanastahili kuulizwa na Waislamu wenye mioyo safi sababu gani wanatumia nafasi yao na fedha yao katika kueneza chuki na uadui kati ya Waislamu. Je, wao hawajatambua hatari inayowanyemelea Waislamu duniani kote ambayo ikiachwa bila kuzuiwa inaweza kuponda Waislamu wote na kufuta hata majina yao katika taarikh ya mataifa? Kwa nii Waislamu wa Kenya wamefunikwa na usingizi mzito kiasi hiki hata wasikione kile kifo kinachosongelea mbele zaidi na zaidi kila siku!

## Husuda ya Mwandishi

Kama tulivyokwisha eleza hapo juu Abdillahi nassir ni mtu aliyepata kusoma sana vitabu vya Jumuiya yetu na anauelewa uhakika wake na anatambua ukweli wake. Na baada ya kutambua hivyo amekata shauri kupinga haki na kuieleza sivyo ilivyo. Na hii ni kwa sababu ya husuda ambayo inamhangaisha roho yake kucha kutwa. Husuda hii inaonekana wazi wazi katika yeye kutuita 'Makadiani' ilhali anafahamu barabara kwamba sisi tunaitwa Waislamu Waahmadiyya. Tumepewa jina hii na kiongozi wetu, Seyidna Ahmad[as], na hili hili tunalitumia katika

maandishi yetu yote na vitabu na magazeti. Na serikalini pia tunajulikana kwa jina hili hili dunia nzima. Hebu someni kwanza maneno ya Abdillahi Nassir aliyoandika kwenye uk. 1 wa kijitabu chake akieleza sababu ya kutuita kwa jina la 'Makadiani'. Ameandika:

> "Hatuweti Wa-Ahmadiyya kwa sababu jina hilo lina maana ya wafuasi wa Mtume Muhammad[saw] ambaye jina lake jengine ni Ahmad kama ilivyo katika aya ya 7 ya Sura 61. Na kwa kuwa wao si wafuasi wa Mtume Muhammad[saw], kama tutakavyoona, ndiyo tukawa hatupendi kuweta kwa jina hilo."

Mmeona ameleta udhuru gani kugeuza jina letu! Amesema 'hatupendi" kuwaita Waahmadiyya kwa jina lao la asili kwa sababu jina hili linawafanya waonekane "wafuasi wa Mtume Muhammad[saw] na yeye hataki tuonekane hivyo. Yaani, sisi tunajiita wafuasi wa Mtume[saw] ila yeye anataka kuhakikisha kwamba sivyo tunavyodai, bali ni kinyume chake.

Wasomaji wapenzi, mnaonaje juu ya kitendo chake hiki cha ujeuri? Kwei Abdillahi Nassir anayo madaraka ya kumpa mtu jina nalopenda yeye? Ikiwa ni hivyo ni yeye tu aliye na madarka haya au watu wengine pia wanweza kumwita Bwana Abdillahi kwa jina wapendalo kumpa? Ikiwa baada ya kusoma maelezo yetu Mwislamu fulani mwema anaona kazi ya Abdillahi Nassir ni kusema uongo na kudanganya watu na kuwapoteza ambayo

ndiyo hasa kazi ya shetani naye hataki kumpa jina Abdillahi bali anamwita Abdishshaitani, je itafaa? Au Mwislamu mwingine wa mwambao anakasirishwa na kazi ya Ansaar Muslim Mission na akapenda kuwapa jina la Ashraar Muslim Mission, je wataridhika nalo? Na hivi ni kwa sababu hao 'Ansaar' walikuwa ni wasaidizi wa Waislamu wakimbizi waliotoka Makka na kufika Madina wakati wa Mtume Muhammad[saw], ambapo hawa wenye kujiita "Ansaar" si wasaidizi, bali ni wapingaji wa Waislamu wa kweli na wanaeneza shari juu yao. Je, majina haya mapya ni maridadi sana kwa hao? Ikiwa sivyo, basi ya nini kumpendelea nduguyo jambo ambalo hulipendi kwa ajili ya nafsi yako. Na twajua sote kwamba Mtume wetu Muhammad[saw] alisema wazi wazi kwamba mtu hawi Mwislamu mpaka ampendelee nduguye yale yale ambayo anayapenda kwa ajili yake mwenyewe. Kama Abdillah hataki kuitwa Abdishshaitani na 'Ansaar' hawapendi kupewa jina la 'Ashraar' (wenye shari) kwa nini wanapenda kutuita jina lisilokuwa letu?

## Uongo Mwingi Umeandikwa

Hautukusema kwa sababu ya chuki ya kuwa mwandishi wa kijitabu **HAKIKA** amekuwa mfuasi wa shetani, bali sasa hivi mtahakikisha kwamba yeye ametumia uongo mwingi makusudi katika utungo wake; na udanganyifu ni kazi kubwa ya shetai. Kwa mfano, katika uk. 7 wa kijitabu chake ameadndika kwamb maneno fulani yamo katika makala iiyochapishwa katika jarida letu liitwalo

**Alfadhl** la Agosti 19, 1916. Kwa bahati nzuri katika maktaba yetu hapa tunalo gazeti hili la Agosti 19, 1916, lakini hatukukuta ndani yake maneno haya wala hamna ndani yake makala iliyoandikwa na Bashir Ahmad, mwanawe Seyidna Ahmad[as]. Wasomaji watukufu, mna haki kamili ya kumwuliza mwandishi huyu kwa nini katunga uongo. Ndiyo alama ya mwislamu safi siku hizi?

Na kwenye uk. 5 wa utungo wake ameandika maneno fulani na akadai kuwa hayo yamo katika ukurasa wa 573 wa kitabu cha Seyidna Ahmad[as] kiitwacho Tajalliyate-Ilahiya. Kwa kuwa mtaalamu huyu hakuona kitabu chenyewe amebuni uongo huu mkubwa kabisa. Ukweli ndio huu ya kuwa kitabu hicho hakina kurasa hata mia. Hakina kurasa hata 50, bali kurasa zake ni 16 tu. Je, hizo nyingine zote kaziona wapi? Na ikiwa ukurasa huo wa 573 haupo, maneno aliyonukuu yamo katika ukurasa upi?

Kadhalika kwenye uk. 2 amesema ya kuwa maneno fulani yanapatikana katika Juzu ya Kwanza ya kitabu Siiratul Mahdi katika ukurasa wake wa 617. Kumbe kitabu hiki kina kurasa 276 tu. Hatujui mwandishi huyu kapotezwa na shetani gani aliyemfunulia maneno haya na kurasa hizi! Kama ilivyoandikwa ndani ya kurani Tukufu (6:113), mashetani nao wanafunuliana wao kwa wao maneno ya uongo ili kupinga haki. Lakini haki inadhihirika mara na uongo kujitenga.

Namna nyingine ya uongo wa Bwana Abdi ni kwamba anadai Seyidna Ahmad[as] kaandika maeneo fulani; kumbe hakuyaandika. Mathalan, kwenye uk. 7 amesema:

(a) "Waislamu wote wanajuja na wanaamini kuwa Muhammad aliyetajwa katika aya ya 30 ya Sura ya 48 ni Mtume Muhammad bin Abdillahi[saw]. Mirza Ghulam Ahmad asema la! Ni yeye..." Huu ni uongo mkubwa sana, tena sana, tena sana! Seyidna Ahamd[as] hakuandika mahali popote kwamba Mtume[saw] hakukusudiwa katika aya hiyo. Si katika kitabu hicho alichotaja huyu Bwana, wala ndani ya kitabu chochote kingine kisichokuwa hicho.

Tena kwenye ukursa huo huo amesmea:

(b) "Waislamu wote wanajua na wanaamini kuwa Mtume Muhammad[saw] ndiye aliyeitwa "rehma kwa viumbe vyote" katika aya ya 108 sura ya 2. Mirza Ghulam Ahmad asema la! Ni yeye!" Huu tena ni uongo mfano wa ule wa kwanza. Seyidna Ahmad[as] hakuandika katika kitabu chake chochte wala katika tangazo lake lolote ya kuwa Mtume wetu Muhammd[saw] siye rehma kwa viumbe vyote. Hakika ni kwamba Bwana abdi alitaka kuhakikisha ukafiri wa Jumuiya ya Ahmadiyya na kiongozi wake mtakatifu, lakini maskini kakosa hoja akawa mwongo mkubwa kuliko waongo wote wa pwani.

Hivyo hivyo, katika uk. 7 akasema tena:

(c) "Waislamu wote wanajua na wanaamini (na hata mwenyewe Mtume Muhammad[saw] amesmea) kuwa makusudio ya Ahmad aliyetajwa katika aya ya 7 ya Sura ya 61, na aliyebashiriwa kuja, ni Mtume Muhammad[saw] lakini hivyo sivyo wasemavyo makadiani. Wao wanasema ati aliyekusudiwa katika aya hiyo ni Mirza Ghulam Ahamd; si Mtume Muhamad[saw]."

Twapenda kutangaza kwa sauti kuu ili kila wa karibu na wa mbali asikie tangazo letu hii ya kwamba hatuamini hivyo wala hatukuandika mahali popote ya kwamba Mtume wetu Muhammad[saw] hakukusudiwa katika aya hii. Tumeandika hapo juu kwamba Bwana Abdi ametaja Jarida letu Alfdhl la Agosti 19, 1916 na kudai ya kuwa maneo hayo yamechukuliwa katika makala ya Hadhrat Mirza Bashir Ahmad[ra] na pia tumeandika kwamba makala hii haimo katika toleo lile maalumu. Lakini sasa tunasema ya kwamba hakuna mwanachama hata mmoja wa Jumuiya hii anayefikiri au anayedai hivyo. Na sababu yake ni kwamba Seyidna Ahmad[as] amepata cheo cha utume kwa sababu ya kumfuata kikwelikweli Mtume wetu Bwana Muhammad[saw] na alipokea ufunuo huu kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

Kullu barakatin min Muhammadin sallallahu 'alaihi wasallama, fatabaaraka man 'allama wa ta'allama.

Yaani kila baraka inayoteremka hutoka kwa Muhammad[saw], hivyo mwenye kufunza (yaani, Mtume Muhammad) ni mwenye mibarka kama alivyobarikiwa mwanafunzi (yaani, Seyidna Ahmad). Ndio kusema, katika hali zote Seyidna Ahmad[as] ni mfuasi na mwanafunzi wa Mtume Muhammd[saw] na amepata kila kitu kwa baraka ya huyu Mtukufu aliye Mfalme wa Milele wa viumbe vyote vya Mwenyezi Mungu. Na jambo hili ameandika mwenyewe Seyidna ahmad[as] katika vitabu vyake na matangazo yake. Bali yeye ameweka kitu hiki mbele ya maadui wa Uislamu na kuwahakikishia kwamba mfuasi wa kweli wa Mtume Muhamma[saw] anapata neema za namana nyingi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambapo mfuasi wa dini nyingine hapati neema yoyote ya kiroho. Na hivyo akahakikisha ubora wa Uislamu juu ya dini zote zie zilizopatikana zamai au zinazopatikana hivi sasa. Na tunatangaza bila hofu ya kushindwa kwamba Bwana Abdi au mpinzani mwingine wa Jumuiya akituonyesha popopte katika vitabu vya Seyidna Ahamd[as] kinyume cha hayo tuliyoandika hapo juu, basi tutakuwa tayari kumpa zawadi yoyote aitakayo. Na ikiwa atashindwa kuona kinyume na hayo, basi tunamwomba asitutangazie uongo kwa sababu ya husuda au kwa kutojua.

Ni kweli Mwenyezi Mungu ametuwekea neema zote na daraja zote za kiroho kwa baraka ya ufuasi wa Mtume Muhammad[saw], lakini Waislamu wa zama hizi hawana habari. Wao wanatazamia ufikaji wa nabii Isa bin

Maryamu[as] ambaye wanamwamini kapaa mbinguni naye ndiye atakayeteremka kutoka huko aje kuwa mtume katika umati wa Mtume Muhammad[saw]. Hili ni kosa kubwa na ni fedheha kwa dini yetu ya Kiislamu kama imani hii ilivyo kinyume na mafundio ya Kurani Tukufu. Bali ni aibu kwa umati wa Muhammad ambao ni umati bora kuliko nyimati zote zingine na juu ya hayo Waislamu hawaoni haya kumpinga mfuasi wa Mtume Muhammad na kumtukuza nabii mwingine aliyetumwa kwa Wayahudi.

Kwa kifupi tunasema kwamba Seyidna Ahmad[as] hakuandika popote pale kuwa Mtume Muhammad hakutajwa katika 48:30 au katika 21:108 au katika 61:7. Wazo hili tunalikataa na kukanusha kwa kila njia tunayoweza kuitumia na kwa uwezo wetu wote. Ni uzushi tu wa maadui ambao wanapenda kuitusi Jumuiya ya Ahmadiyya na kuipaka uchafu.

## Masingizio Yasiyo na Msingi

Hali kadhalika Bwana Abdi amemwita Seyidna Ahmad[as] "mwongo" na "mnafiki" (Mungu apishe mbali) kwa ujinga na husuda na kwa sababu ya kutoelewa maandishi ya Seyidna Ahmad[as], bali twasema kwamba yeye hataki kuelewa maana ya maneno yake. Na ithbati yake ni kwamba yeye amevurugavuruga baadhi ya maneno yaliyoandikwa katika vitabu vya Seyidna Ahmad[as] na kudai kwamba mara yeye anasema mimi nabii na mara anakataa kuwa nabii, na hali pale pale

ameeleza ya kuwa anakataa unabii gani na anajidaia utume wa aina gani.

Katika kijitabu chake (uk. 3) Bwana Abdi ametaja Tablighi Risalat, juzuu ya 10, ukurasa wa 133 na amenukuu tafsiri ya maneno yenye kuhakikisha utume wa Seyidna Ahmad[as] kisha kwenye uk. 5 ameleta tafsiri ya maneno menigne yenye kukanusha dai la utume. Kwa kweli, Bwana Abdi ameingia upotevu wa mbali kwa sababu ya kufuata maandishi ya adui fulani wa Jumuiya Ahmadiyya. Maana maneno yaliyomo ndani ya Tablighi Risaalat, juzuu ya 10, ukurasa wa 133 ni yale yale ambayo tumekwisha tangaza katika kitabu cha Seyidna Ahmad kiitwacho 'Kuondoa Kosa Moja'. Na kitabu hiki kilifasiriwa na kupigwa chapa tangu mwaka 1966 na mpaka wakati huu kimesomwa na watu wengi wa Afrika ya Mashariki. Hatudhani Bwana Abdi alishindwa kukipata na kusoma kitabu hicho maarufu. Ndani ya 'Kuondoa Kosa Moja', Seyidna Ahmad[as] ameeleza jambo hili hili ambalo limemtatiza mtungaji wa 'Hakika ya Ukadiani'. Twaomba wasomaji wetu wasome kitabu kile na kufahamu jibu la swali hili vizuri na kuamua kama Seyidna Ahmad[as] ndiye mwongo na mnafiki au ni Bwana Abdi anayestahili majina haya. Hatuwezi kunukuu kitabu kizima; lakini yafaa tuandike hapa chini machache kutokana na 'Kuondoa Kosa Moja' (uk. 15 na 16) ili kudhihirisha hiyana ya adui wa haki — Bwana Abdi. Seyidna Ahmad[as] anasmea:

"Nami popote nilipokana Unabii wangu au Utume wangu, ni katika maana hiyo tu ya kwamba mimi sikuleta Sheria yoyote mpya wala mimi siye nabii kwa kujitegemea. Lakini kwa njia hii ya kuwa nimepata habari za ghaibu kutoka kwa Mungu nikijipatia fadhili za kiroho kutoka kwa Mtume wangu nimfuataye — Muhammad[saw] — na kwa kupata jina lake na kwa sababu ya wasila wake, mimi ni Mtume na Nabii, lakini bila sheria yoyote mpya. Nami sikukana kamwe kuitwa Nabii wa namna hii bali katika maana hiyo hiyo Mungu Ameniita Nabii na Mtume; wala sikatai hata sasa kuwa kwangu Nabii na Mtume katika maana hii. Na usemi wangu huu:

من نیستم رسول ونیاوردہ ام کتاب[2]

una maana hiyo tu ya kuwa mimi siye mwenye kuleta sheria mpya. Naam, inawapaseni kukumbuka jambo moja, wala msilisahau, ya kwamba juu ya mimi kuitwa kwa neno Nabii na Mtume nimeambiwa na Mwenyezi Mungu kuwa fadhili zote hizi hazikunifikia moja kwa moja bila wasila wowote, bali kuna dhati tukufu huko mbinguni ambayo baraka zake za kiroho nazipokea — yaani dhati ya Muhammad Mteule Sallallahu alaihi wasallam. Kwa sababu ya wasila huo, na kwa kuingia ndani yake, na kwa kupewa

---

[2] Mimi siye mtume wala sikuleta Kitabu.

> jina lake, Muhammad na Ahmad, mimi nimekuwa ni Mtume na pia Nabii — yaani nimetumwa na pia napata habari za ghaibu kutoka kwa Mungu. Na kwa njia hii muhuri wa Khatamun-Nabiyyin umebaki salama kwa sababu nimepata jina hilo kwa njia ya kuwa KIVULI katika kioo cha mapenzi ya Mtume[saw] Na ikiwa mtu yeyote anakasirika juu ya wahyi huu kwamba Mungu kwa nini Amenipa jina la Nabii na Mtume, basi huu utakuwa ni upumbavu wake, kwa kuwa muhuri hauvunjiki nikiwa Nabii na Mtume."

Baada ya kusoma maelezo ya juu, je kuna mtu mwaminifu na mwenye kumcha Mungu anayeweza kumlaumu Seyidna Ahmad[as] na kumwita mwongo na mnafiki na ya kwamba si thabiti katika maneo yake? Ameandika wazi wazi kwamba unabii alio nao yeye una maana gani na huo umepatikana kwa njia gani nao umefuatana na sheria mpya au la. Baada ya kujua hayo yote kuna mtu gani ambaye anaweza kudai kwamba maneno ya Seyidna Ahmad hayaeleweki? Hata leo mtu akituuliza je Seyidna Ahmad ni mwenye kupata utume moja kwa moja, tutakataa. Au akisema, ni Nabii aliyeleta sheria mpya au dini mpya? Tutakataa. Au akidai kwamba Seyidna Ahamd amekuwa badala ya Mtume Muhammad[saw]; pia tutakataa kabisa. Na kwa maana hii hii yeye amesema ya kuwa wahyi wa Mwenyezi Mungu ulianza na Mtume Adam na ukamalizika na Mtume

Muhammad. Yaani wahyi wa kuleta dini mpya na sheria mpya.

Yabainika katika maneno tuliyonukuu hapo juu kwamba MUHAMMAD na AHMAD ni majina matukufu ya Mtume wetu[saw] siyo majina ya mtu mwingine; lakini mwenye kujipoteza katika mapenzi ya Mtume[saw] vile vile amepewa majina hayo kwa sababu yeye amekuwa ni KIVULI chake Mtume[saw]. Na ni dhahiri kuwa kivuli hakifuti mwenye kivuli hicho, bali kinatangaza kuwapo kwake. Na kufutika kwa asili ni kutoweka kwa kivuli pia. Lau kama tufikiri ya kuwa Seyidna Ahmad alijaribu kufuta jina la Mtume[saw], basi kwa mujibu wa maelezo ya juu itamaanisha kwamba yeye alijitahidi kujifuta nafsi yake mwenyewe pia. Kwa maana, kivuli hakitaweza kusimama peke yake baada ya kutoweka kwa asili. Je inaelekea hayo? Hakika ndiyo hii kwamba maadui wa Jumuiya wanafanya dhulma na hiyana pia wanapomlaumu Seyidna Ahmad[as] kwa sababu ya kujipoteza katika mapenzi ya Mtume Muhammad[saw]. Katika kitabu chake kingine maarufu SAFINA YA NUHU vile vile Seyidna Ahmad .a.s. ameleta mfano huo huo wa mtu kujiona ndani ya kioo. Unapojiona sura yako ndani ya kioo, je unafutika na sura yako tu inabaki ndani ya kioo? Au ndani ya kioo unatambua uzuri wako na rangi yako na umaridadi wako? Seyidna Ahamd alizidisha sana ufuasi wa Mtume Muhammad[saw] hata ukakubaliwa katika baraza la Mwenyezi Mungu naye akampa nuru na utume na majina ya Mtume[saw] bila

Mtume[saw] kuyapoteza mwenyewe. Ni kosa kubwa, bali ni upumbavu hasa kufahmau kwamba ikiwa Mwislamu fulani atapewa jina la Muhammad au Ahmad, basi Mtume[saw] ndiye wa asili na ndiye shina na wengine wote wanaomfuata katika nyayo zake ni wanafunzi wake na vivuli vyake. Na Mtume akionekana ndani ya vioo maelfu elfu, basi ni kuenea kwa sifa zake na uzuri wake. Jambo hasa la maana ambalo lafaa kutendwa ni kujipoteza katika huba yake mpaka kila Mwislmau atakasike na kusafika kama kioo hata moyo wake uchukue sura na sifa ya Mtume[saw] kwani moyo usiochukua sura na sifa Mtume[saw] hauna kibali mbele ya mweyezi Mungu. Hii ndiyo maana ya ile aya inayosema kwamb Mtume Muhammad[saw] ni "Mfano Mwema" kwa ajili yetu. Yaani tunatakiwa kumweka daima mbele yetu mpaka moyo wetu uchukue sura yake na sifa zake. Mwenye kupiga picha yako akiisha elekeza kamera yake upande wako sawa sawa anachukua picha yako. Je baada ya yeye kuchukua picha yako unakwenda kumshtaki mahakamani kwa kosa la kukutowesha wewe? Huu ni ujinga dhahiri, Bwana Abdi. Kwa kuwa unamchukia Seyidna Ahmad[as] uzuri wake umekuwa aibu kwako. Na sifa yake imekuwa tusi machoni mwako. Wallahi, Mtume[saw] ametukuka sana sana baada ya kufika kwa Seyidna Ahmad[as] na utukufu huu utazidi na kuongezeka ingawaje maadui wauchukie.

Bwana Abdi angekuwa mwenye roho safi angeongoka baada ya kusoma tu vitabu vya Jumuiya ya Ahmadiyya

kwa Kiswahili. Je, hajasoma kitabu chetu kiitwacho 'Maisha Ya Mtume[saw]'? Je, hajaona kitabu chetu Mtume Muhammad[saw] katika Biblia? Vitabu hivi vinaeleza habari na Maisha na sifa za Mtume gani? Ni habari na sifa za "Makadiani"? Je hajapata kusoma Maombi ya Mtume Mtukfu Muhammad? Ni maombi ya huyu huyu Muhammad[saw] bin Abdillahi au ni maombi ya "Mtume wa Makadiani"? kwa nini amejipumbaza kiasi hiki mpaka watoto wa shule nao watamcheka na kumpa sifa mbaya! Katika kijitabu chake amejivika joho la walimu na amejitolea kujibu maswali ya wanafunzi, kumbe mwenyewe angali anayo akili mbichi hata kuliko vitoto vidogo! Kile chuo ambacho kina waalimu kama Bwana Abdi hakina tumaini la kupata maendeleo; na wanafunzi wake daima watashindwa na kufeli.

Katika Hadithi ya Mtume[saw], mtawala mwema anaitwa Kivuli cha Mungu. Na maana yake ni kwamba sultani au mfalme wa nchi anayewatendea raia wote kwa haki na usawa na anajitahidi kukuza elimu na akili na miendendo na siasa yao, na rehema na huruma yake inawaenea watu wote, ni kama Bwana wao na Mola wao kwani amechukua zile sifa za kiungu ambazo kwake Mwenyezi Mungu ni kwa dhati hasa na kwa viumbe ni kwa kuazima. Mwalimu kama Bwana Abdi akisoma habari hii katika Hadithi atakataa kukubali kwamba Mtume[saw] kanena hivi na atapenda hata kukataa utume wake. Lakini wenye akili wanafahamu mara moja maana za Hadithi kama hii na wanatambua kwamba mfalme

mwema si mwenye kufuta dhati na sifa za Mungu, bali mwenye kuzidhihirisha kwa wanadamu na mwenye kuzithibitisha hata kwa wale wanaomkadhibisha Mungu na kuwapo kwake. Kufuru inapatikana pale tu ambapo kiumbe dhaifu anajivuna na kudai kuwa kakuna Mungu ila mimi tu kama alivyojidaia uungu Firauni, akavuna matunda ya ukafiri wake. Ama Seyidna Ahmad[as], yeye hakujidaia utume wala unabii ila baada ya kuhakikisha kuwapo kwa unabii na utume katika dhati tukufu ya Mtume Muhammad[saw] na akawayakinishia watu wote kwamba kila neema na baraka hupatikana kwa wasila wake yeye tu peke yake. Bali aliongeza kusema kwamba hata manabii waliomtangulia Mtume[saw] kufika duniani walichukua nuru yake Mtume na walifaidi mwongozo uliokuwa sehemu ya mwongozo wa Kurani Tukufu. Tofauti ni hii tu kwamba waliokuja kabla yake waligawiwa nuru hiyo na mwongozo huo na Mungu mwenyewe ambapo wenye kufika baada ya Mtume[saw], kama Seyidna Ahmad, wamepokea moja kwa moja kwa Mtume[saw]. Hivyo umati wa Waislamu safi ukawa bora kuliko wafuasi wa manabii wengine waliotangulia. Hatuna nia kurefusha makala hii kwa kuleta ithbati za jambo hili tokana na maandishi yake Seyidna Ahmad. Yafaa kusoma sehemu ya mwiho kabisa ya kitabu chake ‘Kuondoa Kosa Moja’ inayofuata hapa chini. Asema:

> “Basi, muradi wangu kutoka maandishi yote haya ni huu ya kwamba wapinzani wajinga wananishtaki kuwa ‘Huyo mtu adai kuwa nabii na mtume’. Mimi

> sina madai kama hayo. Mimi siye nabii wala mtume kwa njia wanayofikiria wao. Naam, kwa njia niiyoeleza sasa hivi mimi ni Nabii na Mtume. Basi, yule mtu anishitakiye kwa shari kuwa mimi nadai Uanbii na Utume ni mwongo na mwenye wazo chafu. Njia ya kuwa Buruuz (yaani, mdhihirishaji) imenifanya niwe nabii na mtume; na kwa sababu hiyo, mara kwa mara Mungu amenipa jina la Nabii wa Mungu na Mtume wa Mungu, lakini kwa sura ya kuwa Buruuz, nafsi yagnu haimo katikati bali ni Muhammad[saw], kwa njia hiyo jina langu limekuwa Muhammad na Ahmad. Basi Unabii na Utume haukumjia mwingne; kitu cha Muhammad kimebaki kwa Muhammad, baraka na amani ziwe juu yake.'

Twapena kusema mara ya tena kwamba ufuasi wa aina hii tu ndio unamfanya Mwislamu astahili kuwa mrithi wa Mtumesaw. Hata mawalii wa Kiislamu wamefikia daraja ya uwalii kwa sababu ya utii na ufuasi huo huo. Hadhrat Seyyid Abdul Qadir Jilani, rehma za Mungu ziwe kwake, naye alipata kusema hivi hivi ya kuwa yeye amemrithi Mtume[saw] na akadai kusema; "Kiwiliwili hiki si changu, bali ki kiwiiwili cha babu yangu Mtume Muhammad[saw]. 'Maana yake ni kuwa yeye kajipoteza kabisa katika upendo na utii wa Mtume, hata amekuwa mrithi wake kabisa pamoja na kurithi kiwiliwili chake kwa njia ya majazi. Na ndiyo sababu mawalii nao wanapingwa na masheikh wa kawaida kama Mtume

wetu[saw] alivyopingwa na maadui. Kazi za mawalii na matamshi yao na vitendo vyao vinalingana na kazi na matamshi na vitendo vya Mtume[saw]; lakini wanazuoni vipofu wanashindwa kuvitambua na kuamini na badala ya kujisahihisha wenyewe na kufuata mwendo wa Kiislamu wanawaita mawalii wa Mungu kwa majina mabaya na kuwahimiza Waislamu wa kawaida wawapinge na kutukana. Mawalii wa Kiislamu waliteswa sana na masheikh wa zama zao ingawa leo mawalii hao wanatukuzwa mno na Waislamu hao hao na baadhi yao hata wanakwenda kusujudia makaburi yao. Ni sikitiko kubwa kwamba Waislamu hawashiki njia ya katikati. Pengine wanamtoa mja wa Mungu nje ya Uislamu na kumtangaza kuwa kafiri na pengine humfanya kuwa mungu mdogo na kumwabudu na kumpa wazi sifa za kiungu. Seyidna Ahmad[as] ametumwa na Mwenyezi Mungu ili kuueleza umoja wa Mungu kama ulivyofunzwa na Mtume[saw].

## Dhuluma Kubwa!

Uzushi mwingine mkubwa wa Bwana Abdi ni ule ulioandikwa katia ukurasa wa 5 wa kijitabu chake usemao: "Ushahidi wa kwanza ni kuwa amedai kuwa yeye ni babake Mwenyezi Mungu na pia ni mwana wa Mungu.' Mzushi huyu amejigamba sana ujuzi wake haba na ameshikwa na majivuno kwa kuokota takataka huko na huko hata akaandika kwamba yeye anamwona Seyidna Ahmad[as] kuwa "si Mwislamu kamwe. Ni kafiri hasa!" *A'udhi billahi minashshaitanirrajiim*. Unamwita

Mwislamu mkubwa wa zama zake kwamba ni kafir na ushahidi ulio nao hata hijulikani upo wapi. Tumekwihsa andika hapo mwanzoni ya kwa kitabu cha Seyidna Ahmad[as] *Tajalliyate-Ilahiya* kina kurasa 16 tu; lakini mwogo wa pwani anatoa ushahidi katika ukurasa wake wa 573. Upo wapi ukursa huu na yapo wapi maneo haya ambayo yamefanywa kuwa msingi wa kumtoa Seyidna Ahmad[as] nje ya Dini ya Islamu? Wala hamtakuta maneo haya popote katika maandishi yake yanaomaanisha ya kuwa yeye ni baba wa Mungu au mwana wake. Yeye alitumwa kuvunjilia mbali kila aina ya ushirikina na kufutilia mbali mawazo kama hayo katika nyoyo za wanadamu. Ni husuda tu ya Bwana huyo ambayo inamtuma kuzua mambo yasiyokuwako la ardhini wala mbinguni. Taabu yake mheshimiwa huyo ni kuwa hajui lolote katika Kiarabu wala Kiurdu na bure amejichukulia uzito wa kutoa Waislamu safi katika din ya Islamu.

Ushahidi wake wa pili haumo katika uk. 97 wa *Al-Bushra* ila katika uk. 79 yanapatikana maneo ya Kiarabu ambayo yeye ameshindwa kufahamu maana yake na muradi wake. Neno la kwanza amelifasiri vibaya. Mwenyezi Mungu alimwambia Seyidna Ahmad[as]: *Usalli wa asumu, as'haru wa anaamu*. Neno la kwanza la ufunuo huu *usalli* likitumiwa na mwanadamu maana yake ni 'ninasali'; lakini linapotumiwa na Mwenyezi Mungu huleta maana ya kupeleka rehama. Katika Kurani Tukufu neno hili limetuika juu ya Mwenyezi Mungu

katika aya ya 44 ya sura 33 na hapo limeleta maana ya kurehemu. Tena limetumika mnamo sura hiyo hiyo katika aya ya 57 na pia limeleta maana ya kupeleka rehema. Hiyo ni aya maarufu sana baina ya Waislamu na kwa kawadia tunaifasiri kwa kusema, "Mungu humsalia Mtume wake"; wala hatusemi Mungu anasali. Na neno la pili *asumu* hapa maana yake ni kujizuia kupeleka rehma; kwa sababu *saama* maana yake moja ni 'alijizuia'. Mwenye kufunga saumu vile vile anajizuia na kula na kunywa na badhi ya mambo mengine na tunasema fulani kafunga. Lakini kwa kuwa Mwenyezi Mungu hali wala hafungi chakula, basi maana ya asumu ni kuwa 'najizuia' nisiwarehemu watu fulani, yaani makafiri. Na maana ya sehemu ya kwanza ya ufunuo ni kwamba Mwenyezi Mungu anawarehemu wema na kuzuia rehma yake na waasi.

Sehemu ya pili ya ufunuo pia haikuwa vigumu kueleweka; lakini ujinga na husda vimekutana kumzuia Bwana Abdi asielewe muradi wake. 'Ninakesha' na 'Ninalala' hayakutumika katika maana yake ya kawaida kama yanavyotumika kwa wanadamu, bali maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu analinda waja wake na anawaacha waasi bila ulinzi hata wanashikwa na adhabu kali kali na kuangamia. Yaani, Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa waaminio, na makafiri hawana mlinzi na msaidizi. Kuna aya nyingi za Kurani Tukufu zisemazo kwamba makafiri hawana mlinzi wala msaidizi. Pengine Bwana Abdi hajui matumizi ya lugha na pengine

amejisingizai ujinga ili apate kumtukana Nabii wa Mwenyezi Mungu. Lau kama angesoma kitabu chetu Masomo ya Kiislamu angepata maelezo ya kutosha ya imani yetu juu ya Mwenyezi Mungu na sifa zake. Kadhalika katika maelezo ya aya za Kurani hayakosekani maelezo ya imani yetu kumhusu Mwenyezi Mungu na sifa zake; lakini adui wa haki hana haja ya kupelekeza kwa sababu amekusudia kushambulia na kuaibisha na ktukana.

Mwendo huo huo ameonyesha katika "Ushahidi wa tatu" ambamo amedai kwamba ufunuo wa Seyidna Ahmad[as] ni kinyume na aya ya 53 ya sura ya 20 ya Kurani Tukufu. Maskini huyu kwa kuwa si msomaji wa Kurani, bali anatembezwa ndani yake kama kipofu anavyoongozwa na kipofu mwenzake; basi mara hukosea na mara nyingine husibu. Ni kweli kwamba katika 20:53 Kurani imesema Mungu hasahau. Lakini hajui ya kuwa Mungu anasahau pia. Kama atafunua 7:52 na 20:127 na 32:15 na 45:35 na kusoma tafsiri yake kwa makini ataona ya kuwa Mwenyezi Mungu mwenyewe amesema kwamba atasahau watu fulani. Na maana ya 'kusahau' siyo kama anavyosahau mwanadamu, bali ni kuwatendea watu kana kwamba wamesahauliwa wakati wa kugawiwa rehema ya Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa watu hao walikuwa wanawakadhibisha Mitume na kukataa ishara na aya za Mwenyezi Mungu katika maisha yao ya kidunia, basi Mwenyezi Mungu naye atawatupa katika adhabu kali na kuwaacha humo muda

mrefu kana kwamba wamesahauliwa ndani ya Jahanamu. Je, maelezo haya hayamwingii Bwana Abdi? Ikiwa hakubali maelezo haya basi ni juu yake kutangaza kwamba Kurani imevurugika, mara inasem Mungu hasahau na mara nyingine inasema Mungu husahau.

Hivi ndivyo anatakiwa kueleza ufunuo wa Seyidna Ahmad[as]. Na baada ya kusoma maelezo yetu ya juu atapata kugutuka katika ujinga wake na ataanza kutambua upya maana ya tafsiri za aya za Kurani. Na pia itamdhihirikia kuwa Mungu aliyeteremsha Kurani ndiye huyu aliyemfunulia Seyidna Ahmad[as] katika karne hii; kwa sababu maneno ya Kurani na maneo ya funuo zake yamefanana sana.

"Ushahidi wa nne" wa Bwana huyu (uk. 6) pia ameukusanya katika vitabu vya maadui fulani wa Jumuiya ya Ahmadiyya na amekosea sana. Hakuna kitabu cha Seyidna Ahmad[as] kinachoitwa Wahyul Muqaddas na kwa kuwa hakuna kitabu chenye jina hilo, basi ushahidi wake pia utakuwa hauna miguu ya kusimamia. Kitabu cha pili alichotaja katika ushahidi huu kipo lakini maneo anayodai kuyaona ndani yake hayamo katika ukurasa wake wa 75 wala katika ukurasa wake mwingine. Pengine ni tafsiri mbaya ya maneno fulani au maelezo yaliyopotoka ya ufunuo fulani; hatuwezi kujua. Lakini ni hakika kwamba kiongozi fulani kipofu amempoteza sana kipofu huyu wetu wa pwani hata akagundua yasiyokuwamo ndani ya vitabu

vyetu. Ajabu ni kwamba baada ya kuandika ushahidi wake wa uongo anaulinganisha na maelezo yetu katika ukurasa wa 1060 wa Kurani Tukufu na kudai ya kuwa maelezo yetu ni ya kweli lakini maneno ya Seyidna Ahmad[as] ni ya uongo. Kana kwamb sisi tumeandika ndani ya maelzo ya aya za Kurani amaneo yanayopinzana na maandishi na funuo za Seyidna Ahmad[as]. Hakika yeye huyo amepotea upotevu wa mbali sana. Maelezo aliyoyasoma kwa Kiswahili yamemwongoza na maneno ambayo hakuyasoma kabisa, la kwa Kiswahili wala kwa Kiarabu wala kwa Kiurdu, yamempoteza. Ameteleza pakavu! Juu ya watu kama yeye Mungu amesema, 'Hao ndio walionunua upotevu kwa uongofu; lakini biashara yao haikupata faida, wala hawakuwa wenye kuongoka' (2:17). Ataongokaje mtu huyu anayebuni maneo kisha anayafanya msingi wa kumkataa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Mwendo wake ni maelezo safi ya aya hiyo ya Kurani.

## Dhulumu Nyingine Kubwa

Baada ya kumzulia uongo mwingi Seyidna Ahmad[as], alipenda kuzusha mambo mengine juu ya Waislamu Waahmadiyya vile vile. Anadai kwamba tunapopiga shahada na kusema: "Ninashuhudia kuwa hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu na ninashudhia kuwa Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu" huwa hatumkusudii Mtume[saw], bali twamkusudia Seyidna Ahmad[as] *Astaghfirullahal 'adhiim*. Uzushi gani huu wa

kikafiri! Hatuna la kusema zaidi ya haya: Laana ya Mungu juu ya waongo! Je, moyo wake umekuwa mgumu kiasi hiki hata akazua juu ya imani ya mtu katika moyo wake! Au amekuwa mjuzu wa ghaibu kama Mungu?

Tumekwisha eleza katika kurasa zilizopita kwamba popot pale ndani ya Kurani Mwenyezi Mungu amemtaja 'Muhammad' na 'Ahmad' tunaamini kwamba mwenye kutajwa ni Mtume wetu Muhammad[saw] bin Abdillah bin Abdil Muttalib. Na sasa tunasema kwamba hata katika shahada tunapomtaja Mtume Muhammad[saw], tuna maana ya huyo Mtume Muhammad[saw] bin Abdillahi bin Abdil Muttalib wala siye mwingine minghairi yake. Wala hatumkusudii Seyidna Ahmad[as] wala hatuona haja ya kuunda shahada nyingine ya peke yetu isiyokuwa shahada ya Kiislamu inayojulikana ulimwenguni mwote. Ewe Bwana Abdi, Mungu afunue macho yako na akuokoe katika mtoto wa husuda uliochoma elimu yako na utawa wako na uaminifu wako. Unataka kwetu ushahidi wa namna gani hata ukaamini kwamba katika shahada yetu na katika sala zetu na katika usomai wetu wote wa Kurani tunaposema 'Muhamad' huwa hatumkusudii mwingine yeyote ila Abal Qasim Muhammad[saw] bin Abdillah bin Abdil Muttalib?

Wala hukuelewa maneno ya Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (radhi ya Mungu iwe kwake), uliyoandika kwenye ukurasa wa 8 wa kijitabu chako. Yeye aliulizwa

na mtu mmoja aliyesema ya kuwa ikiwa Seyidna Ahmad ni nabii wa Mungu je mmetengeneza shahada mpya kwa kumtaja yeye Seyinda Ahmad? Swali hili amelijibu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad[ra] kwa kusema kwamba hatuna haja ya kuunda shahada mpya kwa ajili ya Seyidna Ahmad[as]; kwa sababu yeye si mbali na Mtume[saw], bali kuja kwake ni kuja kwa Mtume Muhammad mara ya pili kama ilivyoelezwa ndani ya Sura ya 62, aya ya 4. Hivyo hatuhitaji shahada nyingine. Jibu hili ni kinyume kabisa na maelezo yako na tunaweza kusema kwamba wa mbele umemfanya wa nyuma na wa nyuma umemfanya wa mbele. Mzizi na shina ni Mtume Muhammad[saw] na wafuasi wake wa kweli wanaingia ndani yake kama matawi yanavyoingia ndani ya mti, au kama watoto wa tumbo moja wanavyoingia katika baba yao. Kwenu Waswahili ni rahisi sana kulielewa jibu hili; kwa sababu ninyi mnawapa watoto wenu majina ya baba zenu kwa kudumisha nasaba na ukoo. Kwa mfano, marehemu Sheikh Amri Abedi alimpa mwanye mkubwa jina Abedi ambalo ni lina la babu; lakini hii haina maana kwamba mjukuu ameua jina la babu yake na kumnya'nganya cheo chake, bali imefanywa hivyo kwa kuonyesha uhusiao baina yao na kwa kudumisha kumbukubu ya marehemu babu ambaye amebaki na heshima yake na cheo chake. Ndivyo inavyofanyika katika ulimwengu wa kiroho pia. Mwana wa kiroho hayuko mbali na babake, wala mwanafunzi siye dhidi ya mwalimu wake. Wafuasi

na wanafunzi sio ghairi ya Mtume wao ingawa mwenye chuo daima atabaki Mtume Muhammad[saw] na chuo hicho kitajulikana kwa jina lake na kila ajaye kukiongoza atakiongoza kwa jina lake huyu huyu Mtume Muhammad[saw] ambaye ni Bwana wa waliofika zamani na watakaokuja baadaye. Hakuna jina jingine ila hilo hilo moja tu litakaodumu milele na milele.

## Msiige Mwendo wa Makafiri

Kwenye mwanzo wa kijitabu chake yametajwa baadhi ya mambo fulani yanayohusika na maisha ya Seyidna Ahmad[as] na hali ya afya yake. Hayo si ya maana sana. Kwa sababu kuugua au kusahau ni mambo ya kawaida kwa wanadamu na manabii pia hawaepukani nayo. Mtume wetu[saw] alipata kusahau wakati mwingine na vile vile alipata kuugua. Nabii Ibrahim[as] alikuwa anabishana na makafiri mara akajisikia hawezi akasema, hakika mimi ni mgonjwa (Kurani 37:90). Watu fulani walipoona mwenye kujidaia utume anakula chakula na kutembea barabarani waliona ajabu na kuulizana: "Mtume gani huyu anayekula chakula na anatembea masokoni?" (Kurani 25:8)

Bwana Abdi amejaribu kuiga tabia hiyo ya makafiri wa zamani kana kwamba kusahau na kuugua ni jambo lisilo la kawaida kwa Mitume wa Mwenyezi Mungu. Lakini yeye amepita kidogo hao wa zamani na kujaribu kuchanganya uongo na ukweli ili kustarehesha wenzake zaidi. Ameandika kwamba Seyidna Ahmad[as] aliugua kifua kikuu na kabla ya kufa kwake alikuwa akihara na

kutapika. Ameandika tena, "pia alikuwa na maradhi ambayo yalikuwa yakimsababisha kuanguka na kupotewa na fahamu." Ametia chumvi makusudi, au tuseme amepokea habari za uongo bila kupeleleza kwanza toka viongozi wake wapotevu, kwa kuonyesha hali mbaya sana ya afya ya Mjumbe wa Mungu wa zama hizi na kuwashawishi wasomaji wake wasielekee kumfuata.

Tumekwisha andika kwamba hayo si kweli hata kidogo. Lakini twapenda kumwuliza yeye na wasaidizi wake wanatoa fatwa gani juu ya Nabii Ayub[as] ambaye habari za maradhi yake wamezitaja mufasirina wote wa Kurani na pia Biblia imeeleza habari ya kujaribiwa kwake sana na shetani. Aliugua sana sana muda mrefu hata mwili wake ukaoza na vipande vya nyama vilikuwa vikianguka chini wala hakuna mtu aliyependa kukaa karibu naye. Je, huyu aliyekuwa anatembea na vijidudu katika majeraha yake pia alikuwa Nabii wa kweli wa Mungu au sivyo? Je, baada ya kuugua kwake Mungu Alimtupa na akachukua badala yake mwingine mwenye afya kama Bwana Abdi? Wanaonaje juu ya Nabii Yakubu[as] aliyejaribiwa na mwanaye nabii Yusufu hata akawa kipofu kwa kulia sana na majonzi? Je, Mungu alimtupa baada ya kupofuka kwake? Tunauliza tena je, maadui wa Mtume Muhammad[saw] hawakumsingizia ugonjwa wa kifafa? Je, Mungu alimfukuza Mtume Muhammad eti anaugua kifafa wala hawezi kuwa Nabii wa kweli? Kwanza mtujibu juu ya habari hizi kisha mtafute njia ya kumzulia huyu Nabii wa haki.

Maadui wa Jumuiya hawafahamu kwamba masingizio hayo ni dalili za ukweli wa Seyidna Ahmad[as]. Ni nani aliyewashurutisha waandishi Wakristo waandike hii habari ya Mtume[saw] kuugua kifafa? Ni nani aliyemfanya Bwana Abdi kumlaumu Seyidna Ahmad[as] kwa sababu ya ugonjwa wake wa "kuanguka na kupotewa na fahamu". Ni huyo huyo Iblisi ambaye daima anashindana na Manabii akitumia uongo na masingizio yasiyokuwa ya hakika. Na kwa njia ya masingizio hayo pia Bwana Abdi amehakikisha kwamba kuna uhusiano wa karibu baina ya Muhammad[saw] na Ahmad, maana wamesingiziwa maradhi ya namna moja.

Si hayo tu. Ugonjwa wa Seyidna Ahmad[as] ni dalili ya ukweli wake kwa njia nyingie pia.

Mtume[saw] alimwona Masihi Akher Zamani akiwa amevaa shuka mbili za manjano na wanazuoni wenye kueleza ndoto wameandika kwamba kuonekana na shuka ya kimanjano kunatabiriwa kuugua maradhi. Hivyo, Seyidna Ahmad[as] alihakikisha ukweli wake na kuandika kwamba yeye anaugua magonjwa mawili: wa kwanza ni katika sehemu yake ya juu ya mwili nao ni kichwa kuumwa na kuona kizunguzungu mara nyingine; na wa pili ni katika sehemu ya chini ya mwili nao ni kwenda haja ndogo mara nyingi. Kwa kuwa magonjwa mawili ni alama ya Masihi wa kweli kama ilivyoelezwa katika ndoto ya Mtume[saw]; basi Waislamu hawana budi kumwamini Seyidna Ahmad[as] kwa kuona alama hii nayo

imetimia. Hivi sasa hakuna tumanini kwamba mkisubiri miaka 100 atafika Masihi wa kweli ambaye afya yake itakuwa njema kabisa. Kwa maana, Masihi wa kweli lazima awe anaugua maradhi ya namna mbii na yule ambye ni mzima wa afya hawezi kuwa mkweli. Je, hamna mwongozo kwa ajili yenu katika hoja hii!

Na kwa njia ya tatu vilevile maradhi haya ni sababu ya kudhihirisha ukweli wa Seyidna Ahmad[as]. Ameandka mwenyewe kwamba alikuwa na wasiwasi kwa ajili ya huu ugonjwa wa mkojo, maana husababisha pengine donda baya au kuharibu macho. Na mara Mwenyezi Mungu alimfunulia: Rehema imeteremkia maungo matatau: macho na mengine mawili. Baada ya kupokea ufunuo huu moyo wake ukatulia na macho yake yakabaki mazima mpaka kufariki kwake. Aliishi karibu miaka 80 na muda huu wote hakuvaa miwani wala hakushikwa na ugonjwa mwingine wa macho, bali siku moja kabla ya kufariki kwake alikuwa anatunga makala akiwaita Wahindi wasiitukane dini ya Islamu na wamheshimu Mtume Mtukufu Muhammad[saw]. Ndio kusema, yale magonjwa mawili ambayo ni alama ya Masihi wa kweli yamebaki pale pale bila kuondoka waila ingefutika alama ya ukweli wake; lakini magonjwa hayo hayakuwa na idhini ya kudhoofisha sehemu nyingine za mwili wake. Ni wazi kwamba Mungu ni mwenye uwezo juu ya mambo yote na jambo hili lilithibitika katika maisha yake Seyidna Ahmad[as], hususa kuhusu afya yake. Safari moja aliugua upele wa mikono. Alikuwa

anajikunakuna huku akiwaza moyoni mwake kwamba Mwenyezi Mungu amenipa kazi ya kuongoza wanadamu wote lakini maradhi hayaniachi nifanye kazi zangu. Mara akapata ufunuo: "Sisi Tumechukua dhimma ya afya yako." Kusikia hivi moyo wake ukajaa shukrani ya Mola wake na machozi kulengalenga machoni mwake. Baada ya dakika moja alipofungua macho yake akaona mikono yake mizima kabisa bila hata athari ya maradhi. Ni kweli kwamba taabu na shida hutokea kwa kila mwanadamu; lakini waja wa Mungu wanaona raha sana katika shida hizo kwani wanaona maonyesho ya rehema na msaada wa Mola wao katika kila hali kana kwamba wanamwona Mungu mbele ya macho yao.

Hatuwezi kuandika sana juu ya habari ya magonjwa ya Seyidna Ahmad[as]. Na kila mwenye moyo mwema ataona ishara kubwa katika kazi zake atakapofikiria ya kuwa mtu aliyekuwa na maadui wengi mno, aliyekuwa anashambuliwa toka pande zote, aliyekuwa anashtakiwa mahakamani na maadui, aliyekuwa na mke na watoto na jamaa aliwezaje kutunga vitabu vingi sana na kuandika makala na matangazo chungu nzima na kutoa hotuba mamia katika maisha yake ilihali afya yake si nzuri wala usiku hapati usingizi kwa kufikiria kazi zake na kwa sababu ya kusimama katika ibada. Alikuwa na wageni wengi waliomjia toka sehemu za India na hata toka nje, naye mwenyewe alikuwa anawatumikia na kuwatolea mawaidha na kujibu maswali yao. Mpaka wafuasi wake wakaenea sehemu mbali mbali za India na nje yake katika uhai wake. Je, huu si mwujiza mkubwa

unaoonyesha bila shaka yoyote kwamba Seyidna Ahmad[as] alikuwa anapata msaada maalumu wa Mwenyezi Mungu aliyemtuma kwa kuutumikia Uislamu?

Miongoni mwa Waislamu tunao wanavyuoni wengi mno; wako matajiri kati ya Waislamu; wengine ni wafalme na masultani: hata kati ya Waarabu wako maulamaa na marais wa nchi; lakini kazi iliyofanywa na mtu huyu mgonjwa na maskini inashinda kazi ya Waislamu wengine wote wa dunia nzima kwa ujumla. Je, masheikh wenye afya nzuri na wenye kuoa wake wengi na wenye kumiliki mali na majumba na mashamba wamefanya nini kwa kuuinua Uislamu? Na ikiwa Mola wetu Mtukufu amemjaalia huyu mgonjwa na dhaifu aueneze Uislamu wa kweli katika dunia nzima na kutoka maelezo ya ajabu ya Kurani Tukufu yaliyojaa hekima na maarifa ambayo yanamvuta kila mwenye moyo safi na kumwogofya kila adui wa haki, je tumkimbie eti kwa sababu alikuwa anaumwa kichwa? Hakika nakuambieni, kila mwenye kufikiria hali ya Uislamu na Waislamu katika wakati huu hatakosa kuumwa kichwa na moyo wake kuzama mara. Ni msaada wa Mungu tu unaowalinda watu wema na watawa na kuwajaalia huduma ya dini ya Islamu. Na tunachukua fursa hii kuwaita watu wote wenye nia njema waje kumfuata Kiongozi huyu ambaye alikuwa Mpenzi wa Mungu na ambaye aliwatumikia mataifa yote ili kuwakusanya katika kundi moja na chini ya bendera moja ya kiroho.

## Sharti Mpeleleze kwa Nia Safi

Hatuogopi washindani na wapingaji wala hatushindwi kudhihirisha haki mbele ya mkindani yeyote. Mmekwisha ona kwamba Bwana Abdi wa Mombasa amepotea sana kwa sababu ya kupenda giza na kukimbia nuru. Tumetangaza vitabu na magazeti chungu chungu kwa Kiswahili na tunamshukuru Mungu Bwana huyu hakuweza kupinga jambo hata moja tulilotangaza katika lugah hii tukufu. Yeye ameona nafuu kupinga vitabu vya Kiurdu vya Seyidna Ahmad[as] naye maskini hana ujuzi wa lugha hiyo; akafuata maandishi yaliyojaa udanganyifu ya adui za Jumuiya; akaona mambo chini juu akajitolea kuyapinga. Lakini hili ni kosa lake mwenyewe. Kwa nini kavaa miwani yenye rangi ya manjano hata kila kitu kikachukua rangi hiyo hiyo ya miwani yake? Tunapenda kumwambia kwamba tunataraji kuona Kikao cha Pili baina yake yeye na mwanafunzi wake; lakini tunatumaini safari hii atakuwa mwangalifu sana asifanye makosa yale yale yaliyomtumbukiza katika bahari ya fedheha. Mwenyezi Mungu alimwahidi Seyidna Ahmad[as] akisema: "Nitamfedhehesha kila atakayekusudia kukufedhehesha." Ahadi hii imetima mara nyingi katika uhai wake na baada ya kufariki kwake pia. Mpaka leo ahadi hii ipo na Mungu amesimama imara tayari kutimiza ahadi zake zote.

Na neno letu la mwisho ni: Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote.